

UNITED NATIONS



NATIONS UNIES

**UJUMBE WA KATIBU MKUU WA UMOJA WA MATAIFA
KWENYE SIKU YA KIMATAIFA YA WATU WA ASILI DUNIANI
9 AGOSTI 2023**

Kauli mbiu ya Siku ya Kimataifa ya Watu wa Asili Duniani mwaka huu ni vijana. Tunasherehekea Vijana wa watu Asili, na jukumu lao katika kuleta mabadiliko na kuunda siku zijazo.

Ulimwenguni kote, Watu Asili wanakabiliwa na changamoto kubwa, ardhi na rasilimali zao zikitishiwa, haki zao zikidhoofishwa, na uwezekano wao wa kuendelea kutengwa na kutengwa. Vijana wa Watu Asili wanasaidia kujipigania.

Wao ni viongozi katika harakati za mapambano ya hali ya Tabia nchi duniani. Wanatetea haki na usawa, wanasherehekea tamaduni zao, wanaendeleza haki za binadamu na kuongeza ufahamu wa historia na masuala ya Watu Asili kote ulimwenguni. Na, wakijifunza kutoka kwa wazee wao, wanahakikisha mwendelezo wa tamaduni za Watu Asili, hekima, na utambulisho mbali mbali katika siku zijazo.

Maarifa na mila asilia zimekita mizizi katika maendeleo endelevu na zinaweza kusaidia kutatua changamoto zetu nyingi zinazofanana. Kwa hivyo ni muhimu kwamba vijana wa Watu Asili, wanawake na wanaume, washirikishwe katika kufanya maamuzi. Uchaguzi unaofanywa leo ndio utakaoamua ulimwengu wa kesho.

Kwa hivyo, hebu tuthibitisha tena kujitolea kwetu kudhamini haki za kibinafsi na za pamoja za watu wa Asili vijana pamoja na kuunga mkono ushiriki wao katika midahalo ya kimataifa na kufanya maamuzi. Na kwa pamoja, tujenge mustakabali mwema kwa ajili yetu sote.
